

The Nature Conservancy

# ASILI SASA

## KUBADILI UHIFADHI WAKATI WA CHANGAMOTO ZA DUNIA

RIPOTI YA MWAKA 2020

**“Mwaka uliopita tulijifunza, kwa uwazi zaidi kuliko awali, namna afya na ustawi wetu ulivyounganishwa na afya ya sayari.”**

—JENNIFER MORRIS, AFISA MKUU MTENDAJI

**Juu ya jarada:** Mwonekano kutoka juu wa Hifadhi ya Taifa ya Wood-Tikchik ya Jimbo la Alaska, hifadhi kubwa zaidi ya serikali ya Marekani yenye takriban ekari milioni 1.6. Maji ya hifadhi hutiririkia kwenye Ghuba ya Bristol, sehemu kubwa zaidi duniani ya uvuvi wa samaki aina ya Samoni. Mwaka 2020 wasimamizi wa shirikisho walisitisha kwa muda mipango ya mgodi mkubwa kwenye vyanzo vya ghuba, kutokana na juhudi za vikundi vya wenyeji, jamii za wavuvi, wahifadhi na wengine. © Michael Melford

# Kuimarisha mustakabali wa siku za usoni kwa asili ya sasa

**MNAMO MEI 2020,** Nilijiunga na Shirika la Uhifadhi wa Mazingira yaani The Nature Conservancy au TNC kama Afisa mkuu mtendaji — mojawapo ya siku za kujivunia na za kufurahisha zaidi katika kazi yangu ya miaka 25 ya uhifadhi. Kwa kweli, wiki chache za kwanza hazikwenda kama nilivyotarajia. Au miezi ya kwanza. Janga la COVID-19 liliibuka, na kusababisha uharibifu kwa familia, mifumo ya huduma za afya na uchumi duniani kote. Takriban mwaka mmoja baadaye, wengi wetu tunaendelea kufanyia kazi nyumbani na kuzingatia umbali wa kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine baina ya marafiki, jamaa na wapendwa.

Ingawa ilikuwa sura ya kwanza yenye changamoto kwangu nikiwa TNC, shirika ambalo nilikuwa nalipenda sana na nilitarajia kufanya kazi nalo siku moja, tuliweza kugushi uhusiano na kufanya maendeleo makubwa.

“Nilikutana” na maelfu ya jamaa na mamia ya wadhamini na wafuasi kupitia Zoom badala ya ana kwa ana. Wenzangu na Mimi tulijifunza juu ya ushirikiano wetu na wenyeji kutumia moto kuirejesha misitu yenye afya kupitia mazungumzo na picha, bila kuhisi mvuke kutoka kwenye moto uliodhibitiwa. Tulisherehekea uanzishwaji wa Hifadhi mpya ya Taifa ya Fishers Peak, Jimbo la Colorado yenye ekari 20,000 bila kutazama milima mirefu. Na tulijifunza jinsi ya kupanda miti ya mikakao kupitia apu ya ujumbe wa kijamii pamoja na wapandaji huko Brazil bila kushikilia mche mikononi mwetu au kupata harufu ya ardhi yenye unyevu ya msitu oevu ulioko karibu. Unaweza kujifunza zaidi juu ya miradi hii na mingine ya TNC kupitia kurasa zijazo.

Changamoto nyingi zilizoukumba mwaka 2020 - janga la dunia, joto kali kupita kiasi, moto na vimbunga, na hesabu za muda mrefu zenye mifumo ya kibaguzi na wito wa usawa - zinaendelea kuathiri maisha yetu. Lakini mwaka 2020 pia ulijulikana kama mwaka wa uvumilivu, uthabiti na ubunifu. Dunia ilikaa pamoja kushughulikia shida kwa njia mpya, kwa kasi na ushirikiano usiyo wa kawaida. Hapo awali jamii ya kisayansi haikuwahi kamwe kutumia akili na rasilimali nyingi kwa pamoja kwa kasi hivyo. Utengenezaji wa chanjo mpya zenye nguvu chini ya mwaka mmoja umeongeza matumaini ya kuchukua hatua za haraka juu ya vitisho vingine duniani, kama vile udharura wa hali ya hewa.

Mwaka uliopita tulijifunza, kwa uwazi zaidi kuliko hapo awali, jinsi afya na ustawi wetu ulivyounganishwa na afya ya sayari yetu. Mwezi Mei 2020, Shirika la Afya Duniani lilichapisha ilani yake ya *Uponyaji wa Afya kutokana na COVID-19,* ambayo inapendekeza kulinda na kuhifadhi asili kama kipaumbele cha juu. Kulinda asili kunasaidia uchumi, kunaleta hewa safi na maji na chakula bora, na kunaweza pia kupunguza baadaye hatari ya miripuko ya magonjwa ya kuambukiza, ambayo sayansi inatuambia kwa sehemu yanasababishwa na ukosefu wa makazi na mabadiliko ya hali ya hewa.

Kwa kweli, janga hili lilidhihirisha nguvu ya asili katika kuponya—sio tu kupitia uvumbuzi wa kiasili kama kilimo cha kisasa kinachozingatia uhifadhi, upunguzaji wa hewa ya ukaa na vyanzo vya nishati safi kama upepo na jua lakini pia katika kusaidia watu wengi kuishi katika dunia yenye taabu. Mnamo mwaka 2020, ziara za maeneo ya asili na hifadhi ziliongezeka kwa kiwango kikubwa, mauzo ya vifaa vya kutembelea maeneo ya nje na ya baiskeli yaliongezeka, kutafuta na kuangalia ndege mwituni kuliongezeka, na kupanda milima na matembezi kwenye sehemu za asili kuliongezeka. Kote duniani, watu walianzisha tena uhusiano wao na asili na walitafuta faraja nje ya makazi yao.

Kwa imani hii, natafakari juu ya yote ambayo Shirika la TNC liliweza kutimiza kwa msaada wa washirika, wafuasi na uongozi wetu wa kujitolea mwaka 2020 - na natazamia miaka kumi ya matumaini kwenye uhifadhi wa asili duniani kote. Nina matumaini kwamba tunaweza kutumia ukakamavu na uthabiti ambao sote tulipata mwaka huu mgumu katika kujenga kwa pamoja mustakabali mzuri.

Kila la heri,



© ALEX SNYDER/TNC

**Jennifer Morris**
Afisa Mkuu Mtendaji,
The Nature Conservancy

## MABADILIKO TUNAYOHITAJI KATIKA KIPINDI CHA MABADILIKO YANAKUJA SASA, WAKATI WA CHANGAMOTO ZA KIPEKEE.

Yote tunayokabiliwa nayo leo yanatutaka tufanye mabadiliko ya kweli na ya kudumu ambayo yatatuongoza kwenye ulimwengu wenye mapya yanayowezekano kwa watu na asili. Kwa TNC, hii ndio changamoto ya wakati wetu. Pia ni wakati ambao umetuandaa kwa miaka 70 ya uzoefu na kujizatiti. Sasa ni wakati wa kuchukua hatua; sasa ni wakati wa kuibadilisha dunia yetu na kulinda ardhi na maji vinavyotegemewa na maisha yote.

Miamba ya matumbawe ya Karibiani ni hazina ya dunia. Sasa basi, kwa mara ya kwanza kabisa, mataifa yanapata ramani zenye viwango vya juu vya makazi haya ya chini ya maji, kutokana na jitihada za TNC na washirika wake wa sayansi. Wanasayansi walitumia picha kama hii kutoka sehemu inayoitwa Jardines de la Reina huko Cuba, zilizonaswa kupitia "kikundi cha nyota" cha satelaiti zaidi ya 200, kutengeneza ramani ambazo zinaweza kusaidia kuachapisha uharibifu kutokana na vimbunga, kutambua vipaumbele vya urejesho na kupanga ulinzi wa siku zijazo.

© PLANET LABS INC



Hifadhi mpya ya Fishers Peak yenye ekari 19,200 inatazamana na Trinidad, Colorado, ambapo fursa mpya za burudani zitaleta neema ya kukua kwa uchumi wa eneo husika.



© CAMERON DAVIDSON

# Hifadhi Mpya ya Taifa Inaubadili Mji wa Colorado

**KWA MIONGO, WAKAZI KATIKA** mji wa zamani wa uchimbaji madini wa Trinidad, Colorado, walikuwa wakiwaona vijana wakiuhama kwenda mbali kupata fursa za ajira. Mwaka 2017, Meya Phil Rico aliamua kuwasiliana na TNC na Mfuko wa Ardhi ya Umma yaani The Trust for Public Land (TPL) akiwa na mpango wa mabadiliko: Je, mashirika yanaweza kusaidia kulinda ranchi ya jirani kwa kujikita kwenye kuubadilisha mji kuwa kitovu cha mafanikio cha burudani za michezo ya nje? Mwaka jana, maono hayo yalitimia ambapo eneo hilo lilibadilishwa kuwa hifadhi ya taifa yenye kilele cha mlima wenye urefu wa futi 9,633.

Baada ya TNC na TPL kununua ranchi ya ekari 19,200 kwa msaada kutoka kwa Great Outdoors Colorado, taasisi hizi mbili zilisaidia Hifadhi na Wanyamapori wa Colorado kupata mali ya dola milioni 25.4 na kuibadilisha kuwa Hifadhi ya Taifa ya Fishers Peak. Hii ina uhakika wa kuwa sehemu ya utalii wa nje ikiendana na maajabu ya asili ambayo tayari yanachangia dola bilioni 62 kwenye uchumi wa taifa. Hifadhi hiyo ina spishi 900 — ikiwa ni pamoja na wapiti, paka pori mwekundu na kozi kipanga— na inasaidia kupata usharoba wa wanyamapori kutoka Milima ya Sangre de Cristo kwenda kwenye ukanda wa nyasi za nyanda za juu.

"Kwa kupanga malengo ya kiikolojia na ya burudani kutoka ghorofa ya chini, tutajitahidi kuonyesha jinsi matokeo madhubuti ya uhifadhi yanachangia jamii inayostawi kiuchumi, wakati wote huku tukiunganisha vizazi vijavyo na asili," anasema Matt Moorhead, mshauri wa ushirikiano wa uhifadhi wa TNC huko Colorado.

# Mkakati wa Dunia wa Kuinusuru Mito

**LENGO** Mito huleta uhai kwa wote. Mfumo mpya wa Kudumu wa TNC wa Utunzaji wa Mto unasaidia maji safi na salama kutiririka.

**WAKATI BALKANA** ikiwa ni kitovu cha mito mingi inayotiririkia huko barani Ulaya, ukanda huu umelengwa miaka ya hivi karibuni kwenye mipango ya kuendeleza mabwawa mapya ya maji na miradi mingine ya maji. Licha ya vitisho hivyo, juhudi za TNC katika ukanda huo mwaka jana zilisaidia kulinda mito miwili: maji ya samawati ya Mto Zeta unaopatikana Montenegro na, kaskazini, Mto Krupa huko Kroatia, ambayo hupita kwenye korongo lenye mwinuko na lenye miamba.

Serikali mbili zililinda mito kwa kutumia njia mpya ya TNC ya ushirikishwaji wa jamii ya utunzaji wa mito inayojulikana kama mfumo wa Kudumu wa Utunzaji wa Mto. Ukiwa kwenye Sheria ya Mito ya Porini na yenye Mvuto Marekani, mfumo huo unaleta njia mpya za sera ambazo zinaweza kusaidia utunzaji wa maji safi duniani. Hii ni muhimu kwa sababu mito ndio chanzo cha bayoanuai nyingi duniani lakini, cha kushangaza, haitunzwi sana kwenye mifumo ya asili ya Dunia.

Mafanikio ya Balkana yatasaidia kuridhiwa kwa mfumo huu kwenye nchi nyingine pia.

Askari pori kwenye Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Randilen nchini Tanzania husaidia jamii zao kwa kuwalinda wanyamapori.




© ROSHNI LODHIA


## "Kama maaskari pori hawa wangepoteza kazi zao wakati wa janga, kimsingi tungepoteza mwelekeo."

Mafanikio ya **Alphonce Mallya** wa The Conservancy juu ya **Mfuko wa TNC wa Mgogoro wa Hifadhi za Wanyamapori Afrika,** uliochangisha dola milioni 2.5 kutoka kwa wafuasi wa TNC. Mfuko wa dharura uliweka maaskari pori wapatao 950 kushika doria katika hifadhi za wanyamapori nchini Kenya, Namibia, Tanzania na Zambia – wakipunguza ufadhili kwenye uhifadhi wa utalii wa kiikolojia kutokana na kupungua kwa wageni kwa 90%. Wengi walikuwa na wasiwasi kuwa mgogoro ungeweza kuathiri jamii husika na hifadhi za wanyamapori, kikwazo kwa uhifadhi shirikishi ambao ungewaacha wanyamapori katika hatari kubwa zaidi kutokana na ujangili.

# Kumaliza Mkwamo wa Uchangiaji kwenye Bayoanuai

**BAYOANUAI ZA DUNIA** ziko katika hatari ya kutoweka. Kiwango cha kutoweka kwa viumbe kinazidi kuongezeka na mabadiliko ya hali ya hewa sasa yanazidi kuwa tishio. Kupungua kwa bayoanuai kutakuwa na athari kubwa kwa watu, kama vile kukosekana kwa maji safi na vyanzo vya chakula kupungua. Kwa mfano, tishio la kukosa wachavushaji kunaweza kusababisha anguko la pembejeo za kilimo linalokadiriwa kuwa dola bilioni 217 kwa mwaka. Jarida jipya, *Financing Nature*, lililochapishwa na taasisi ya Paulson, Chuo Kikuu cha Cornell na TNC, linaelezea mabadiliko kwenye sera na kanuni za fedha ambazo zingeweza kusaidia uwekezaji mpya kwenye sekta binafsi unaoweza kulinda asili na bayoanuai.





Asili huleta **CHAKULA** mezani petu na **MAJI** kwenye mabomba yetu. **NJIA MBELENI** inahitaji tuwe wabunifu **SASA.**

Kuanza uzalishaji wa mazao yenye kuhitaji maji kidogo— kama shamba hili la ngano Arizona— kunaweza kuwa na uendelevu wa chakula na maji.

Ukiwa umesheheni mimea aina ya Msafsafi na pamba pori, Mto Verde huko Arizona unakatisha sehemu murua kwenye jangwa.



## Kuanza Uzalishaji wa Mazao yenye uhitaji mdogo wa Maji kunatumia Maji Chini ya 50% na Kuchochea Fursa Mpya

**LENGO** Wakulima wanahitaji maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na kukuza uchumi wa ndani. TNC inathibitisha kuwa uchaguzi mzuri wa mazao kwenye ukame wa Magharibi unaweza kuleta maji zaidi kwa watu na asili.

**KATIKA BONDE LA MTO VERDE HUKO ARIZONA,** mabadiliko ya dhati kwenye ardhi yameleta athari chanya kusudiwa: katika maji yenye kuleta uhai ya Mto Verde. Ukitiririsha maji yake kutoka nyanda za juu katikati mwa Arizona, Verde yenye urefu wa maili 190 na viunga vyake vya mto vyenye mimea aina ya Msafsafi na pamba pori ni chemchemi ya maisha. Mto pia unamwagilia mashamba ya ukame na kusambaza jamii kwa maji ya kunywa. Hivi karibuni, mto umetumiwa vibaya sana kiasi kwamba sehemu zimekauka wakati wa majira ya joto, na kutishia uwezekano wa baadhi ya mashamba na maisha ya wanyamapori, ikiwa ni pamoja na spishi mbili za samaki zilizo kwenye hatari ya kupotea.

Ili kushughulikia tatizo, TNC, pamoja na washirika wa ndani katika biashara na kilimo, walipendekeza mabadiliko ambayo yalionekana kuwa na uwezo wa kufanya yasiyowezekana: kuokoa maji ya thamani wakati huo huo wakikuza mazao yenye soko na kuhamasisha ukuaji wa sekta mpya katika uchumi wa eneo hilo. Kwa kifupi, TNC ilifanya kazi na shamba kubwa zaidi katika ukanda huu kuwa na mwelekeo wa kulima ngano, ambayo hutumia nusu ya maji ambayo yangetumika kwa ajili ya mazao yenye kutumia maji mengi kama alfalfa na mahindi. Na TNC ilisaidia kwa kampuni mpya kusindika ngano kwa ajili ya bia.

Kwa miaka mitatu tu, kuhamia kwenye uzalishaji wa ngano ya kiwango cha juu kumeleta mafanikio makubwa kwa watengeneza pombe ya kienyeji, kumeokoa galoni milioni 425 za maji — za kutosha kujaza mabwawa ya kuogelea yenye ukubwa wa Olimpiki zaidi ya 600 — na kuufanya Mto Verde utiririke.

THIS PAGE AND OPPOSITE: © ANDREW KORNYLAK

### "Mwokozi mkubwa wa maisha."

Hivi ndivyo **Laura Brown**, mvuvi wa kome wa New Hampshire, anafikiria juu ya **hatua za TNC** katika kurudisha matumbawe ya kome na wavuvi wanaounga mkono walioathiriwa na kupungua kwa mauzo wakati wa janga hili.

Mradi huu, ukiongozwa na TNC na Mfuko wa The Pew, uliingia ili kuunda soko jipya kwa zaidi ya wavuvi 100 wa kome ambao walijikuta wakihangaika wakati COVID-19 iliposababisha migahawa na mahitaji ya kome kuyumba.

Wavuvi wa chaza katika majimbo saba wanaweza kuuza kome wao wa ziada wenye afya kwa mradi huo, uitwao SOAR —kifupi cha maneno yenye maana ya Kusaidia Ufugaji na Urejeshwaji wa Kome— ambao huwapandikiza katika maeneo ya karibu na miamba ya urejesho. Kome mmoja anaweza kuchuja galoni 50 za maji kwa siku, na mwamba mzima wakome unaweza kuwa muhimu kwa afya ya ghuba na maeneo ya bahari. Maeneo ya kome yenye kuvutia — biashara za familia zilizodumu kwa muda mrefu na kuanza tena hivi karibuni — sio tu hutoa faida hizi za kiikolojia lakini mara nyingi huchangia pia kwenye uchumi wa vijijini. Kukamilisha lengo la SOAR la kununua kome milioni 5 kwa kipindi cha miaka miwili kunamaanisha kwamba wazalishaji wataweza kubaki juu wakati juhudi za muda mrefu za kurejesha miamba husika zinasimamiwa vyema.

# Ulinzi wa Samoni na Jadi kwenye Ghuba ya Bristol, Alaska

**LENGO** Asili husaidia uvuvi wa samaki aina ya samoni wakati wa kiangazi katika mito ya ghuba ya Bristol huko Alaska. TNC inajizatiti kulinda kwa muda wote ardhi na maji ya ghuba kutokana na mipango ya kujenga mgodi kwenye vyanzo vya maji.

**KATIKA GHUBA YA BRISTOL,** mbinu ya jadi ya kuishi kwenye vijiji vya Wazawa wa Alaska imekuwa ikitegemea daima maji safi na kurejea kwa samaki mwitu kila mwaka. Samaki hawa ni idadi ya mamia ya mamilioni, zaidi ya mahali pengine popote duniani, na hivyo kuifanya Ghuba ya Bristol kuwa tumaini bora la mwisho kwa tamaduni na uchumi uliofungamana moja kwa moja na mavuno endelevu ya samoni mwitu. Hatahivyo mito yake inayojulikana, maziwa na makazi ya dubu na ayala bado hayana walinzi wa kudumu dhidi ya vitisho kama vile Mgodi wa Kokoto uliopendekezwa, ikimaanisha kwamba maisha yao ya baadaye hayako salama kutokana na madhara. Sayansi ya TNC kwa muda mrefu imesaidia mashirika ya wazawa na tasnia endelevu ya uvuvi wa kibiashara, ambayo, kwa pamoja mwaka 2020, yalisaidia kusimamisha mgodi kwa muda katika kampeni endelevu inayoendelea leo. Kupitia umoja huu mpana, TNC inaendeleza ushindi huu na kutetea ulinzi wa kudumu kisheria pamoja na uwekezaji muhimu katika kuimarisha uchumi wa eneo hili na mamlaka ya eneo hili —hatua zote za mabadiliko katika kujenga mustakabali mzuri wa watu na asili kufungamana vyema na Ghuba ya Bristol.


↗ Nahodha wa biashara ya uvuvi na wafanyakazi wa meli huleta mavuno ya samaki aina ya samoni mwitu ghuba ya Bristol.
→ Mila zisizopitwa na wakati huendelea kutumika na Wenyeji, ambapo kurudi kwa samoni husababisha watu kukutana kuvua kwa pamoja samaki na kuzihifadhi katika nyumba za kificho zenye moshi.



“Mila juu ya samoni mwitu zisizopitwa na wakati za Ghuba ya Bristol bado zinaishi na ni salama — kwa sasa. Lakini hatuwezi kubweteka. Tunachofanya baadaye, kwa wakati huu, kinatoa picha ya baadaye kwa vizazi vijavyo.”

—STEVE COHN, MKURUGENZI WA THE NATURE CONSERVANCY JIMBO LA ALASKA

© BRIAN ADAMS (BRISTOL BAY); © JOÃO RAMID (AMAZON)



Kuvuna maganda ya kakao ili kutoa chokoleti kunaweza kusaidia upandaji miti katika msitu wa Amazon na kutoa mapato thabiti kwa wakulima wadogo.



# Apu ya Simu ya Kiganjani yawahamasisha Wakulima Kuokoa Msitu wa Amazon

**KWENYE MSITU WA AMAZON YA BRAZIL,** wakulima wadogo wamesababisha upotevu wa takriban theluthi moja ya msitu mnene kwa kukata miti kwa ajili ya kupata mashamba na malisho ya ng’ombe kwa ajili ya kujikimu na kupata mapato. Lakini tangu mwaka 2012, TNC na serikali ya jimbo la Pará wamekuwa wakitoa msaada wa kitaalam na mafunzo kuhamasisha wakulima kupanda miti ya kakao - chanzo cha chokoleti - kupanda upya miti iliyoharibiwa na kutoa chanzo endelevu zaidi cha mapato. Hatahivyo, mwaka jana, msimu wa mavuno ulipokaribia, COVID-19 iliikumba Brazil, na kufanya mafunzo ya ana kwa ana kuwa hatari sana. Shirika la TNC liliamua kutumia apu ya ujumbe mfupi kwa kupitia mitandao ya kijamii kurusha video kwa wakulima wapatao 250 kwa wakati ili kusaidia mavuno.



Moshi hufuka wakati wa msimu wa joto huko Australia. Mabadiliko ya tabianchi yanachangia moto huu wa msimu.

**MABADILIKO YA TABIANCHI** ndio changamoto kuu kwetu kwa sasa. Makabiliano ni ya **KIDUNIA**, ni ya **ENEO HUSIKA**, na yanaanza **SASA**.

© ANDREW MERRY/GETTY IMAGES

# Zawadi ya Dola Milioni 100 yaipa motisha TNC Kukabiliana na Hali ya Hewa

**JUHUDI ZA KIUNGUNDUZI ZA TNC** za kuleta ufumbuzi wa hali ya hewa ya asili zilipokea msaada mkubwa wa zawadi ya dola milioni 100 kutoka Mfuko wa Dunia wa Bezos. Zawadi hiyo inafadhili kazi ya hali ya hewa maeneo mawili muhimu—majimbo ya kilimo ya Punjab na Haryana huko India, pamoja na Ukingo wa Emerald wa pwani ya Washington, British Columbia na Alaska. Fedha hizo pia zinasaidia juhudi za kuleta ufumbuzi wa hali ya hewa kwa kiwango kikubwa. Zawadi hii, ya pili kwa ukubwa kupokewa na TNC, inaanzisha kazi yetu ya kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa kote duniani.

### INDIA

**Changamoto:** Wakulima kuchoma mabaki ya mazao kuandaa mashamba yao tayari kwa msimu wa upanzi na kusababisha uzalishaji wa hewa ya ukaa na uchafuzi wa hewa katika miji jirani.

**Suluhisho:** Kuanzisha mbinu mpya za kisasa za kilimo—pamoja na kulima bila kutifua—humaliza mahitaji ya kuchoma, huokoa maji, huongeza mapato ya wakulima, hukuza afya ya mchanga na kuhifadhi hewa ya ukaa.

### UKINGO WA EMERALD

**Changamoto:** Misitu yenye joto la Ukingo wa Emerald hutunza hewa ya ukaa kwa kiwango kikubwa zaidi duniani, lakini misitu hii iko kwenye hatari ya kutoweka.

**Suluhisho:** Kuhifadhi misitu minene ya pwani kwa kushirikiana na watu wa Mataifa makubwa huheshimu maono ya uwakili unaoongozwa na wenyeji wakati wa kutunza misitu kama maghala ya hewa ya ukaa.



© RALPH A. CLEVENGER/TANDEM STOCK

Ufadhili kutoka Mfuko wa Dunia wa Bezos utasaidia kuhakikisha ulinzi wa muda mrefu wa ekari 250,000 za msitu wa zamani, makazi ya wanyamapori kama dubu, huko Columbia, Canada na kusaidia kazi ya hali ya hewa katika Ukanda wote wa Emerald.

> **"Asili inabadilika na hatuwezi kuizuia, kwa hiyo tunatakiwa kutafuta njia ya kuilinda wakati inabadilika."**

**Dkt Mark Anderson**, mkurugenzi wa TNC wa sayansi ya uhifadhi, sehemu ya mashariki mwa Marekani, **kuhusu zana mpya ya TNC iliyokamilika ya Kuainisha na Kuunganisha Mazingira.** Kwa maana fulani, zana hiyo hutumika kama ramani ya "barabara kuu za asili na viunga vyake" inayofunika theluthi moja ya Marekani Bara. Ramani hai inaonyesha ambapo spishi za mimea na wanyama zina nafasi nzuri ya kukabiliana na vitisho vya hali ya hewa vinavyoongezeka — na kupata maeneo mapya ya kupigia simu nyumbani. Tafiti zinaonyesha kuwa kila muongo mimea na wanyama wanahama kwa takriban maili 11 kaskazini na futi 36 Kwenda juu katika mwinuko kwa kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa, na kuufanya mradi huu kuwa nyenzo muhimu ya uhifadhi.

Sayansi ya TNC inaonyesha jinsi ya kulinda ardhi ya asili wakati vyanzo vipya safi vyenye nguvu kufikia malengo 0muhimu ya hali ya hewa.




## Zana za Uhifadhi zinaweza Kusaidia Kutimiza Malengo ya Mkataba wa Paris ya Nishati Safi Mara 17 Zaidi - Bila kuathiri Ardhi Asilia

**KUJENGA-NJE YA** Nishati jadidifu iko mbioni kuanza kutumika, na kwa kasi isiyo ya kawaida. Lakini vyanzo vingine vya nishati safi, kama vile upepo na mitambo mikubwa ya umeme wa jua, huhitaji maeneo makubwa ya ardhi. Wanasayansi wa TNC wanaonyesha jinsi mataifa yanaweza kufanikisha malengo ya nishati safi duniani wakati wa kutunza ardhi asilia.

Ramani hai ya maingiliano ya Upepo wa Hifadhi ya Tovuti ya TNC inasaidia sekta kuharakisha mipango wakati inaongoza maendeleo ya miundombinu mbali na makazi nyeti katika Milima Mikuu, na mikakati mipya inafanya vivyohivyo kwa nishati ya jua huko California, Nevada na West Virginia.

Nchini India, chombo kipya cha SiteRight cha TNC kinathibitisha kifaa muhimu cha kupanga kwa sekta inayopanuka haraka ya nishati mbadala ya nchi. Anasema Dhaval Negandhi wa TNC, mchumi wa ikolojia, “Kama hamfikiri juu ya athari hizi, zinakuwa mizozo ambayo inazuia na kupunguza kasi ya mradi wenu.” Pamoja na malengo makuu ya kitaifa ya nishati safi nchini India, tasnia haiwezi kumudu ucheleweshaji wa ujenzi, kwa hiyo zana sahihi ya TNC inatoa njia ya nishati safi kwa siku zijazo.

## Kuheshimu Ukarimu wa Wafadhili kwa Msitu wa Shukrani

**KUPANDA MTI MMOJA** ni tendo la tumaini na imani katika kile kinachokuja. Katika eneo la Serra da Mantiqueira kule Brazil katika Msitu wa Atlantiki ulio hatarini kutoweka, TNC inapanda miche, mmoja baada ya mwingine, ikileta maisha mapya kwenye milima iliyoathirika na ukataji miti. Kupitia kila mti uliopandwa, Msitu wa Shukrani unamea na kwenda juu —kuenzi ukarimu wa mawakili wa kujitolea wa TNC.

Katika kuwashukru wafadhili wetu, TNC inastawisha msitu huu mahali pa uhitaji na uwezekano mkubwa. Mto upitao chini kwa chini huko São Paulo na Rio de Janeiro, watu wanategemea misitu ya Mantiqueira kuhifadhi na kuchuja maji ambayo hufanya maisha yawezekane.

Msitu huu wa Shukrani si wa juhudi ya mmoja. Ni sehemu ya kampeni kama msukumo wa TNC wa Kupanda Miti Bilioni moja, ikianza kama zawadi na kisha, kama mbegu, inakua alama kwa vizazi vijavyo.

Kupitia Msitu wa Shukrani, TNC na washirika wanasaidia kurejesha misitu ya ukanda huu, iliyosimamiwa na wafuasi wetu, kwa sababu tunaamini kwamba tendo lenye nguvu la kupanda mti ni uwekezaji katika sayari siku zijazo.

© IAN SHIVE/TANDEM STOCK

© KILIII YÜYAN

Zima moto akisimamia mpaka wakati wa uchomaji moto wa kimila kwenye Mafunzo ya Moto huko Yurok, California mwaka 2019.



## Wenyeji Warejesha Moto kwenye Mandhari

**WENYEJI,** kama vile watu wa Karuk, Yurok na Hupa wa California ya leo, wamekuwa wakichoma moto kwa malengo na kwa kuudhibiti usienee kote kwa milenia. Walakini katika nchi nyingi zilizoendelea, moto huu wa asili, na faida zake za kiikolojia, ulipotea sana karne ya 20 mara nyingi kwa sababu ya sera kandamizi juu ya moto wa mwituni.

Kudhoofika kwa afya ya misitu na nyasi nyingi sasa kunadhihirisha gharama za muda mrefu za kuondoa moto kwenye mandhari yaliyoundwa na wasimamizi wa moto wa Asili. Kuzuia moto wa kiwango cha chini kunaweza kusababisha moto mkubwa mwituni — wakati mwingine maafa —ambao huathiri afya ya binadamu, hudhuru asili na kuhatarisha maisha ya jamii.

Kupitia kuunganisha Australia, Canada na Marekani, TNC inasaidia juhudi za wazawa za kufufua matumizi ya moto wa asili katika muktadha wa leo. Katika mipango ya mafunzo ya moto ya TNC Amerika ya Kaskazini, ambayo husaidia kuchoma takriban mara 600 kwenye ekari 100,000 kila mwaka, sasa tunasaidia kuwezesha au kufadhili warsha, kubadilishana mafunzo na kufanya mafunzo ya jamii ambayo yanasaidia juhudi za wenyeji kuleta faida za uchomaji moto kitamaduni kwa watu pia kwa mandhari.

> “Bila kushiriki kwa wazi katika tamaduni zetu za uchomaji moto, tunapoteza utamaduni wetu.”
>
> —BILL TRIPP, MKURUGENZI WA SERA YA MALI ASILI NA MAZINGIRA KWA KABILA LA WAKARUKI

**MWAKA WA FEDHA ULIOPITA,** uongozi wa TNC haukutoa wakati na umakini mkubwa kushughulikia na kukabiliana na athari za janga la dunia la COVID-19 kwa wafanyakazi wetu, kazi ya uhifadhi na utafutaji fedha ambalo lilitikisa huduma za afya duniani, taasisi za kitamaduni na kifedha kwa kiasi kikubwa. Katika kukabiliana na janga hili, TNC ilifanya mabadiliko mengi muhimu ya jinsi tulivyofanya biashara—kufunga ofisi zetu duniani, kuwawezesha wafanyakazi wetu zaidi ya 4,000 kutumia njia ya mtandao kwenye kazi na kukuza ubunifu ili kuendelea kushirikiana na wafadhili na wafuasi wetu.

Menejimenti yetu ilipitisha njia inayofaa ya kihafidhina ya usimamizi wa gharama katika mwaka huo ambao haujawahi kutokea, ikirudi nyuma wakati masoko yalipoporomoka kipindi cha kipupwe kwa kupunguza matumizi kwa 20%, kupunguza mishahara mikubwa hadi 15%, kuzuia nyongeza zote za malipo, kupunguza wafanyakazi wetu na kusitisha karibu safari zote.

Kwa bahati nzuri, hatua za kuchochea uchumi zilizochukuliwa na uchumi unaoongoza kote duniani zilisaidia kuweka mizani sawa ya masoko ya fedha na kuwezesha wafuasi wa TNC kuendelea kuchangia katika shirika kwa ukarimu. Kwa kweli, kwa ushirikiano na ukarimu wa wafadhili na wafuasi wetu, mwaka wa fedha 2020 kilikuwa bora zaidi kwetu kwa rekodi kubwa kwenye mapato ya juu. Kumalizika kwa Kampeni yetu ya Ulimwengu na fursa kadhaa za kipekee za kutafuta hela, pamoja na kumalizika kwa Shindano la MacArthur juu ya Hali ya Hewa na kuongeza michango kadhaa mikubwa kusaidia kazi ya TNC na Blue Bonds ya hali ya hewa, ilisaidia kukuza ukuaji huu mkubwa.

Licha ya changamoto zilizosababishwa na janga hili, tuliweza kuifikia zaidi dunia na kuonyesha uwezo wetu katika sayansi na uhifadhi—pamoja na kuhamasisha karibu dola bilioni 1 kwenye mtaji—kufanikisha faida kubwa za uhifadhi.

Tulipata fursa zaidi katika Mwaka wa Fedha 2020 kutathmini muundo wa jalada letu la uwekezaji na kutekeleza mikakati kadhaa ya kuboresha afya ya jalada. Hii ilisababisha utendaji kwenye jalada ambalo lilizidi vigezo vyetu vilivyowekwa.

Katika kutazamia na kutumaini chanjo kutolewa kawaida, tunaona biashara iliyo na mizania yenye nguvu ya kipekee, ikiendelea kuungwa mkono na wafadhili na wachangiaji, wafanyakazi na utamaduni uliofanyiwa majaribio na shida wakati wote ili kuendeleza dhamira yetu kabambe ya kuhifadhi ardhi na maji ambayo maisha yote hutegemea.



© BILL MARR/TNC

**Leonard Williams**
Afisa Fedha Mkuu

MALIPO NA MICHANGO BINAFSI KWA AINA YA WAFADHILI

- **36%** MASHIRIKA YA FEDHA
- **24%** WATU BINAFSI
- **23%** MAOMBI
- **4%** MIFUKO & MENGINEYO
- **13%** MASHIRIKA YA MISAADA

UFANISI ENDELEVU

- **68.5%** PROGRAMU
- **17.9%** JUMLA & UTAWALA
- **13.7%** UKUSANYAJI WA FEDHA & UANACHAMA

*Kwa miaka ya fedha inayoishia Juni 30, 2020 na 2019 (kwa maelfu)*

| **MSAADA & MAPATO** | **2020** | **2019** |
|---|---|---|
| Madeni na michango binafsi | 783,245 | 595,311 |
| Michango ya Serikali | 126,423 | 127,764 |
| Jumla ya Madeni & Michango | 909,668 | 723,075 |
| Kipato kutokana na Uwekezaji | 78,252 | 93,994 |
| Vipato vingine | 93,178 | 139,021 |
| Mauzo ya ardhi na tuzo | 148,943 | 99,464 |
| **Jumla ya Msaada & Mapato** | **1,230,041** | **1,055,554** |

| **GHARAMA & MANUNUZI YA ARDHI & MAKUBALIANO** | | | % ya kila dola iliyotumika **2020** | **2019** |
|---|---|---|---|---|
| Shughuli na hatua za uhifadhi | 536,341 | 520,142 | 53.0% | 49.2% |
| Manunuzi ya ardhi ya hifadhi na makubaliano | 156,210 | 232,085 | 15.4% | 22.0% |
| Jumla ya gharama za programu za uhifadhi & Manunuzi ya Ardhi ya Hifadhi & makubaliano | 692,551 | 752,227 | 68.5% | 71.2% |
| Za jumla na za utawala | 180,679 | 161,705 | 17.9% | 15.3% |
| Kutunisha mfuko na uanachama | 138,127 | 142,548 | 13.7% | 13.5% |
| Jumla ya huduma wezeshi | 318,806 | 304,253 | | |
| **Jumla ya Gharama & Manunuzi ya Ardhi ya Hifadhi & Makubaliano** | **1,011,357** | **1,056,480** | | |
| **Matokeo Ghafi—Msaada & Mapato juu ya Gharama & Manunuzi ya Ardhi ya Hifadhi & Makubaliano** (1) | **218,684** | **(926)** | | |

| **MALI, MADENI & MUHTASARI WA MALI GHAFI** | | |
|---|---|---|
| Ardhi ya Hifadhi | 2,150,851 | 2,128,184 |
| Makubaliano ya uhifadhi | 2,386,747 | 2,288,383 |
| Uwekezaji kwa ajili ya miradi ya uhifadhi | 941,950 | 774,397 |
| Uwekezaji salama | 1,334,391 | 1,309,105 |
| Uwekezaji uliopangwa | 315,736 | 322,475 |
| Mali & vifaa (ghafi kwenye kushuka kwa thamani) | 152,334 | 141,972 |
| Mali nyingine (2) | 588,371 | 745,774 |
| **Jumla ya Mali** | **7,870,380** | **7,710,290** |
| Akaunti lipwa na madeni yaliyojitokeza | 145,425 | 219,410 |
| Noti zilizopokelewa | 338,123 | 398,491 |
| Madeni mengine (3) | 420,291 | 375,754 |
| Jumla ya mali ghafi | 6,966,541 | 6,716,635 |
| **Jumla ya Madeni & Mali Ghafi** | **7,870,380** | **7,710,290** |

(1) Haikukusudiwa kuwakilisha kuongezeka kwa mali ghafi.

(2) kimsingi ni pamoja na pesa taslimu, ahadi za tuzo za baadaye, madeni yaliyoletwa chini ya makubaliano ya kukopesha dhamana, noti zinazopokewa, mali iliyoruhusiwa kutumika na kuwekeza kwenye ardhi na mali nyingine.

(3) Kimsingi ni pamoja na mapato yaliyoahirishwa, yanayolipwa chini ya makubaliano ya kukopesha dhamana, deni pangwa, deni la hati na madeni mengine.

**Kumbuka:** Takwimu zinazoonekana zilizoonyeshwa katika muhtasari fedha zimetokana na taarifa za fedha za 2020 na 2019 ambazo zimefanyiwa ukaguzi na kupata maoni yasiyofaa.

Taarifa kamili za fedha, zilizokaguliwa za 2020 na 2019 za TNC zinaweza kuonekana kupitia **nature.org/AnnualReport** au kuombwa kutoka TNC kwa namba **(800) 628-6860** au **+1 (703) 841-5300 (800)**.

**Mwenyekiti wa bodi**

**Frances A. Ulmer**
Kiongozi Mwandamizi
Kituo cha Belfer
Shule ya Harvard Kennedy
*Anchorage, Alaska*

**Makamu mwenyekiti**

**Sen. William Frist**
Mshiriki na Mwenyekiti
Cressey and Co.
*Nashville, Tennessee*

**Afisa Mkuu Mtendaji**

**Jennifer Morris**
Shirika la Uhifadhi wa Mazingira (TNC)
*Arlington, Virginia*

**Mweka Hazina**

**Joseph H. Gleberman**
Mkurugenzi Mkuu
Shirika la The Pritzker
*New York, New York*

**Katibu**

**Brenda Shapiro**
Mdhamini wa Muda Mrefu wa TNC
Na Mhifadhi
*Chicago, Illinois*

**Wajumbe**

**Amy Batchelor**
Mkurugenzi Mkuu
Anchor Point Foundation
*Boulder, Colorado*

**John Bernstein**
Mshirika
Generation Investment
Management
*London, UK*

**Michelle J. DePass**
Rais na Afisa Mkuu Mtendaji
Mfuko wa Kumbukumbu ya Meyer
*Portland, Oregon*

**Harry R. Hagey**
Mwenyekiti Mstaafu
na Afisa Mkuu Mtendaji,
Dodge & Cox
*Menlo Park, California*

**Margaret A. Hamburg**
Katibu Mambo ya Nje
Chuo cha Taifa cha Udaktari
*Washington, D.C.*

**Shirley Ann Jackson**
Rais
Chuo cha Rensselaer
*Troy, New York*

**Sally Jewell**
Katibu Mstaafu wa Mambo
ya Ndani wa Marekani
*Seattle, Washington*

**Nancy Knowlton**
Mwenyekiti wa Sayansi ya Viumbe
Bahari Makumbusho ya Taifa
ya Historia Asilia Emerita Smithsonian
*Brooksville, Maine*

**Edwin Macharia**
Mshirika Kiongozi Mkuu
Kampuni ya Ushauri ya Dalberg
*Nairobi, Kenya*

**Claudia Madrazo**
Msanii na Mhifadhi
*Mexico City, Mexico*

**Craig O. McCaw**
Mwenyekiti na Afisa Mkuu Mtendaji
Makampuni ya Eagle River
*Kirkland, Washington*

**Ana M. Parma**
Mtafiti
Kituo cha Taifa
Patagónico CONICET
*Puerto Madryn, Argentina*

**Douglas B. Petno**
Afisa Mkuu Mtendaji wa Benki
ya Biashara JPMorgan Chase
*New York, New York*

**Vincent Ryan**
Mwenyekiti
Schooner Capital LLC
*Boston, Massachusetts*

**Kent J. Thiry**
Afisa Mkuu Mtendaji Mstaafu
na Mwenyekiti Mtendaji
DaVita
*Denver, Colorado*

**Kevin Weil**
Makamu Rais wa Product
Novi
*Menlo Park, California*

**Ying Wu**
Mwenyekiti
China Capital Group
*Beijing, China*



**MIPANGO YA ZAWADI NA MILIKI**

# Kuhakikisha Mustakabali wa Asili

Shukrani kwa maelfu ya watu wanaofikiria mbele ambao wameacha alama katika asili kwa kulikumbuka Shirika la TNC katika mipango yao ya mali isiyohamishika. Mwaka uliopita pekee, tuzo zilizopangwa kwa TNC zilifikia zaidi ya dola milioni 170. Msaada huu usio na kifani unadhihirisha kwamba TNC inaweza kuendelea kuifanyia ubunifu na kubadilisha kazi yetu ya uhifadhi duniani ili kupata kesho yenye kuwakutanisha watu na asili.

**nature.org/GiftAndLegacy | legacy@tnc.org | (877) 812-3698**

**TUNASHUKURU KWA MSAADA WA WAFADHILI WETU WOTE UNAOENDELEA.**
Ili kutoa mchango utakaoleta matokeo ya haraka juu ya asili sasa,
tafadhali tembelea ***nature.org/Donate***.

**Kuhifadhi ardhi na maji ambayo hutegemewa na maisha yote.**

Ili kupata taarifa zaidi juu ya kazi za Shirika la TNC kwenye nchi 72 na majimbo yote 50 ya Marekani, tembelea **nature.org**.

© 2021 The Nature Conservancy.

**WOCRJ 21007**